Mwongozo wa Sheria za Haki za Makazi za Vermont

Jua haki zako na mambo unayoweza kufanya kuhusu ubaguzi unaohusiana na makazi



Imetengenezwa na Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont
Ilisasishwa Desemba 2022

Kila mtu anastahili kuishi katika ulimwengu usio na ubaguzi.

Muhtasari huu kutoka kwa Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont utakusaidia kuelewa:

Haki zako za kisheria zinazohusiana na makazi

Jinsi ofisi yetu huchunguza ubaguzi wa makazi



Mambo unayoweza kufanya ukipitia ubaguzi wa makazi

Kitabu hiki cha mwongozo kimeandikwa kwa madhumuni ya kielimu. Wasiliana na ofisi yetu iliyo katika Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont(hrc.vermont.gov) ili kujifunza zaidi au kuuliza maswali.

Kuelewa Sheria za Haki za Makazi

Ubaguzi katika mifumo ya makazi nchini Marekani ulianza zamani sana. Ubaguzi huu bado unadhuru watu leo.

Pia ndiyo sababu kuna sheria nyingi za haki za kitaifa, jimbo na za mitaa zinazolinda watu leo.

Je, nani anapaswa kufuata sheria za haki za makazi?

Mtu yeyote anayehusika katika kukodisha, kuuza, kugawa maeneo, au kufanya maamuzi ya kifedha yanayohusu nyumba lazima afuate sheria hizi. Watu hawa ni pamoja na:

- Wamiliki wa nyumba, wasimamizi wa mali, na wafanyikazi wao
- Mashirika ya nyumba
- Mawakala wa mali isiyohamishika, wakadiriaji, benki, na watu wengine wanaohusika katika mchakato wa kuuza nyumba
- Wajumbe wa bodi ya ugawanyaji wa maeneo mbalimbali

Wakati mwingine, watu wanaotekeleza majukumu haya hawaelewi sheria kikamilifu, na wao husema au kufanya mambo yanayoweza kuwa kinyume cha sheria.

Wakati mwingine, watu wanaweza kujua kwamba matendo yao ni ya kibaguzi.

Haijalishi ni SABABU gani mtu hafuati sheria za haki za makazi. Ikiwa mtu hafuati sheria za haki za makazi, una haki.

Je, nani analindwa na sheria za haki za makazi za Vermont?

Kwa ujumla, sio halali kisheria kubagua watu katika masuala yanayohusiana na makazi kwa sababu zozote hizi:

- Mbari au rangi
- Jinsia, hisia za kimapenzi, au utambulisho wa kijinsia
- Umri
- Ikiwa mtu ameoa au hajaolewa
- Dini
- Nchi ambayo mtu anatoka au kwa sababu mtu huyo hakuzaliwa nchini Marekani au katika jimbo la Vermont
- Ikiwa mtu anaishi na watoto wenye umri wa chini ya miaka 18
- Ikiwa mtu ana ulemavu (na, kwa mfano, anaishi na mnyama wa kumsaidia kufanya shughuli za kila siku)
- Ikiwa mtu anapata usaidizi wa umma (kama vile Sehemu ya 8, kwa mfano)
- Ikiwa mtu ni mwathirika wa unyanyasaji, unyanyasaji wa kingono, au kufuatwa fuatwa

Sheria hizi HAZIMAANISHI kuwa wataalamu wa masuala ya makazi lazima wakodishe au wauzie mtu yeyote nyumba. Wataalamu wa masuala ya makazi bado wanaweza kuwaomba watu wachukue hatua kama vile kukamilisha ukaguzi wa wadhamini au kujaza ombi. Wataalamu wa masuala ya makazi wanaweza kuhakikisha kuwa wapangaji wanaweza kulipa kodi.

Lakini HAWAWEZI kuwatendea watu tofauti kwa sababu ya mbari, rangi, jinsia, n.k. (vikundi vilivyoorodheshwa hapo juu).

Je, hatua gani ni kinyume cha sheria?

Hapa kuna baadhi ya mifano ya ubaguzi wa makazi katika maisha halisi tukizingatia hali ya mtu wa kundi linalolindwa:

	Nini sio halali kisheria...	**Hii Yaweza Onekana Kuwa...**
	Kukataa kukodisha au kuuzia (au kuzungumza kuhusu kukodisha au kuuzia) mtu nyumba	"Nadhani ungependa nyumba iliyo katika eneo lingine."
	Kutaja bei tofauti au kufanya makubaliano tofauti	"Samahani - bei ni $1500 kwa mwezi." "Lakini rafiki yangu alikodisha nyumba kubwa zaidi kwa $1200." "Oh, um…"
	Kutangaza au kusema kwamba watu fulani pekee ndio wanaokaribishwa	"Inafaa kwa wanandoa wachanga au waseja wasio na watoto!" "Samahani - sichukui Sehemu ya 8."
	Kusema kuwa huwezi kuzuru mahali ilihali wengine wanaweza kuzu	"Haipatikani ..." "Lakini rafiki yangu amekupigia simu, na ukasema inapatikana."
	Kutaja mikopo, kupanga bei, au kufanya makubaliano tofauti ya kifedha	"Nyumba hii ina thamani ya $200,000." "Lakini nyumba iliyo chini ya barabara ilikadiriwa kuwa $250,000, na yetu ni nzuri zaidi."
	Kumtisha mtu ili akuuzie au akukodishie nyumba	"Vipi, labda ni wakati mzuri sana wa kuuza. Hujui kitakachotokea usipopokubali ofa hii."
	Kutomruhusu mtu kushiriki katika shughuli za kawaida za mali isiyohamishika kama vile kukagua orodha iliyochapishwa	"Samahani - sina orodha iliyochapishwa ya mali isiyohamishika ya nyumba hiyo. Acha nikuletee orodha ya mali zingine zilizo katika eneo tofauti."
	Kuamua jinsi ardhi inavyotakiwa kutumika	"Hatukubali kupanga nyumba hii kwa watu wanaosaidiwa kuacha ozoelevu kwa sababu kuna watoto wengi katika eneo hilo."

Pia unalindwa unapozungumza dhidi ya ubaguzi wowote na sheria za haki za makazi!

Ulinzi kwa Waathiriwa wa Unyanyasaji, Unyanyasaji wa Kingono, au Kufuatwa fuatwa

Watu ambao wamekuwa waathiriwa wa unyanyasaji, unyanyasaji wa kingono, au kufuatwa fuatwa wana haki za ziada katika makazi yanayohusiana na mambo waliyopitia.

Hakuna yeyote anayeweza kueleza au kutumia taarifa inayohusu mpangaji au mtu anayeruhusiwa kuishi mahali fulani na kutumia hali yake kama mwathirika wa vita vya nyumbani:

- Kumsumbua
- Kumlipizia kisasi kwa ajili ya kujua na kutumia haki zake
- Kumlazimisha ahame
- Kujaribu kumfanya apeane mali zake

Hatua zozote hizi sio halali kisheria.

Ulinzi kwa Watu wenye Ulemavu

Watu wenye ulemavu wana haki za ziada zinazohusiana na makazi.

Je, ulemavu ni nini? Katika sheria hizi, ulemavu unarejelea hali hizi zozote:

- Mtu ana matatizo mwilini au akilini yanayomzuia kufanya shughuli moja au zaidi ya maisha kama vile kuona, kutembea, kuwasiliana, kujifunza, n.k.
- Mtu ana historia au matukio ya matatizo yanayomzuia kufanya shughuli moja kuu au zaidi za maisha
- Mtu anatendewa tofauti na mtu anayefikiri kuwa ana matatizo (haijalishi ikiwa mtu huyo ana matatizo hayo)

Kuna aina tofauti za ulinzi kwa watu wenye ulemavu katika makazi kama vile kurekebishiwa hali na mazingira ili iwafae.

	Ni nini...	Mifano...
Kurekebishiwa hali	Kubadilisha, kurekebisha, au kukubali sheria au sera tofauti ili mtu mwenye ulemavu atumie nafasi kama mtu mwingine yeyote.	• Kuruhusu mnyama wa kumsaidia mtu mwenye ulemavu, hata kama kuna kanuni inayosema "wanyama vipenzi hawaruhusiwi". • Kutoa njia mbadala ya kujaza maombi • Kuweka eneo la kuegesha gari ambalo mtu mwenye matatizo ya kutembea anaweza kufikia
Kurekebishiwa mazingira	Kuruhusu mtu mwenye ulemavu anayeishi mahali (au atakayeishi hapo) kukarabati jengo hilo au maeneo ya watu wote ili aweze kutumia nafasi kama mtu mwingine yeyote.	• Kuweka ubao wa mtu kushikilia anapokuwa bafuni • Kujenga mteremko wa kushukia au kupandia ili mtu aweze kufikia langoni • Kuongeza njia ya pekee inayozuia hewa iliyo ndani ya nyumba isipotee ikiwa inawezekana.

Vidokezo vichache kuhusu kurekebishiwa mazingira:

- Unaweza kumwomba mhudumu wa nyumba akusaidia kulipia gharama ya ukarabati, lakini si lazima akubali kuilipia gharama hizo (vinginevyo, mtu mwenye ulemavu anayeomba kufanya ukarabati lazima alipie gharama za ukarabati wowote)
- Wamiliki wa majengo HAWAWEZI kuwaomba watu wenye ulemavu watoe amana ya ziada ya usalama inayohusiana na ukarabati
- Ikiwa inawezekena, mwenye jengo anaweza kumwomba mpangaji ahakikishe kuwa nyumba itengenezwa ilivyokuwa awali kabla ya ukarabati wakati anaamua kuhama

Je, kuna mambo mengine yanayoruhusiwa katika sheria za haki za makazi?

Ndiyo, kuna baadhi ya hali maalum ambapo sheria tofauti hutumika.

Umri

Baadhi ya majengo ya makazi yanaruhusiwa kusema kwamba lazima watu wawe na umri fulani ili waweze kuishi hapo:

- Maeneo ya watu wenye umri wa miaka 62 na zaidi
- Maeneo ya watu wenye umri wa miaka 55 na zaidi (na yamejengwa mahususi kwa ajili ya wazee) huku zaidi ya 80% ya watu wanaoishi hapo wakiwa wenye umri wa miaka 55 au zaidi.
- Mpango wa serikali kuu au ya jimbo uliotengenezwa kwa ajili ya watu wazima na shughuli zake ni za kuwasaidia watu wazima

Hali inayoruhusiwa hapo juu ni: watu waliohamia kwenye jengo mnamo au kabla ya Julai 1, 1989, wanaweza kuishi katika jengo lenye masharti ya umri. Wakazi wapya lazima watimize matakwa ya umri.

Vile vile, hakuna mtu anayehitajika kisheria kukodisha au kuuza nyumba kwa mtu aliye na umri wa chini ya miaka 18 katika jimbo la Vermont.

Idadi ya Wanafamilia

Wataalamu wa masuala ya nyumba hawawezi kubagua familia zilizo na watoto.

Wanaweza kuiambia familia kuwa hawawezi kukodisha nyumba ikiwa wanafamilia ni wengi kuliko wanaoruhusiwa na sheria. Kwa mfano, mji unaweza kuweka amri kwamba idadi ya watu wanaoruhusiwa kuishi katika nyumba fulani ni watano kwa sababu ya mfumo wa maji taka.

Mashirika ya Kidini

Baadhi ya mashirika ya kijamii yanaweza kuruhusiwa kuwa na masharti ya watu wanaoweza kuishi katika jengo kulingana na dini zao.

Mali Ndogo za Kukodisha

Ikiwa nyumba iko katika jengo lenye vitengo vitatu au vichache na mmiliki au mwanafamilia wa karibu wa mmiliki wa nyumba anaishi katika mojawapo ya vitengo, hahitaji kufuata sheria za haki za makazi.

Jinsi Tume Inavyofanya Kazi

Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont ni idara katika serikali ya jimbo. Tuna wafanyakazi 6 wanaoshughulikia masuala yanayohusiana na ubaguzi katika makazi, maeneo ya umma na ajira serikalini. Kundi la makamishna 5 tofauti huteuliwa na gavana kwa kipindi cha miaka 5. Tume hii inasimamia shughuli za idara.

Huwa:

- **Tunashiriki taarifa** ili watu waelewe haki zao
- **Tunachunguza** ubaguzi wa makazi na aina zingine za ubaguzi, pia
- **Tunashirikiana ili tupate suluhu** kukiwa na tukio la ubaguzi
- **Tunaandikisha kesi dhidi ya wahudumu wa nyumba** wanaokiuka haki za watu
- **Tunajulisha maafisa wa serikali ya jimbo** kuhusu masuala haya
- **Tunashirikiana na maafisa wa serikali kubadilisha sheria** ikiwa inahitajika

Mbona uandikishe malalamiko ya ubaguzi wa nyumba?

Kila mtu ana haki ya kuishi katika ulimwengu usio na ubaguzi.

Kwa kuripoti ubaguzi wa makazi, unaweza:

- **Kusaidia kukomesha ubaguzi** kwa ajili yako, familia yako, marafiki zako na jamii yako
- **Kusaidia kufanya mabadiliko ya kweli** – wakati mwingine, unaweza kupata pesa kwa ajili ya mambo uliyopitia au kuboresha jinsi biashara zinavyofanya kazi
- **Kuwasaidia maafisa wa serikali kutunga sheria mpya au kutekeleza sheria za sasa vizuri zaidi** wakiwa na taarifa hizi

Je, mchakato huo unafanyaje kazi?

Ikiwa mtu anafikiri kuwa amepitia ubaguzi unaohusiana na makazi, anaweza kuwasilisha malalamiko kwa idara yetu. Hivi ndivyo inavyofanya kazi:



Hapa kuna maelezo machache muhimu unayohitaji kujua kuhusu kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi wa makazi:

- Hatuwezi kulazimisha mtu yeyote alipe faini au fidia LAKINI tunaweza kusaidia kwa mazungumzo ya kutatua mzozo wako kwa kuzungumzia kuhusu maafikiano.
- Tunakusanya taarifa tunapochunguza mambo yanayoweza kukusaidia mahakamani ukiamua kuandikisha kesi baadaye
- Mchakato haukugharimu chochote, na hauhitaji wakili

Kwa kuwasilisha malalamiko, unaisaidia jamii yako kuwa mahali salama na panapowakaribisha watu wote.

Mambo ya Kufanya Ukipitia Ubaguzi wa Makazi

Anza kwa kufuatilia taarifa zote zinazohusu hali hiyo kadri uwezavyo. Kwa mfano:

Hifadhi ujumbe na maandishi ya barua pepe

Hifadhi matangazo au vipeperushi vyovyote

Andika maelezo haraka uwezavyo (tarehe, nyakati, na mambo yaliyosemwa)

Je, kinachofuata ni nini?

Ukipitia ubaguzi wa makazi, una chaguzi tofauti za jinsi unavyoweza kushughulikia tukio hilo. Unaweza:

1. Kuzungumza na wakili ikiwa unafikiri unaweza kutaka kuandikisha kesi yako mwenyewe (Chama cha Wanasheria wa Vermont kina tovuti ya kutafuta mawakili)
2. Kuzungumza na Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont na uandikishe ripoti ili ofisi yetu iweze kufanya uchunguzi

Mnaweza pia kuandikisha kesi yenu NA kuwasilisha malalamiko katika ofisi yetu.

Kuchunguza ubaguzi wa makazi kunaweza kuwa mchakato mrefu, lakini ni muhimu sana kuripoti ubaguzi unapotokea.

Je, ninaandikisha vipi malalamiko kuhusu ubaguzi wa makazi? Au kuuliza tu maswali?

Kuna njia kadhaa unazoweza kutumia kuwasiliana nasi ili uandikishe malalamiko ya ubaguzi wa makazi au kuuliza maswali yanayohusiana na jambo hili:

Jaza fomu ya malalamiko mtandaoni:
hrc.vermont.gov/complaint



Zungumza na wafanyakazi walio katika Tume ya Haki za Kibinadamu ya Vermont:
1-800-416-2010 (Bila malipo VT) au 1-802-828-1625

Tuma barua pepe yenye maswali kwenye:
human.rights@vermont.gov

Asante kwa kusaidia kukomesha ubaguzi wa makazi katika jamii yako!